

Maswali

1. Nani alikuwa mwana mpendwa wa Yakobo?
2. Yakobo alimpa Yusufu nini?
3. Yusufu alikuwa na ndoto mbili gani? Zilikuwa na maana gani?
4. Ndugu zake walipanga kumfanyaje Yusufu?
5. Nani alikuwa mzuri kuliko wengine?
6. Walifanyaje Yusufu?
7. Nini ilifanyika wakati Reubeni hakukuweco?
8. Yusufu alipelekwa wapi?
9. Ndugu zake walifanyaje kanzu la Yusufu?
10. Yakobo alifikiria nini ilifanyika kwa Yusufu?

Majibu

1. Yusufu alikuwa mwana mpendwa wa Yakobo.
2. Yakobo alipea Yusufu kanzu la rangi nyingi.
3. Miganda ya ndugu zake zilimwinamia. Jua, mwezi na nyota zilimwinamia. Ndugu zake watamwinamia.
4. Ndugu zake walipanga kumuua.
5. Reubeni alikuwa mzuri kuliko wengine.
6. Walimtoa kanzu na wakamtupa kwa shimo.
7. Wafanya biashara walikuja. Ndugu zake walimuuza kama mtumwa.
8. Yusufu alipelekwa Misri.
9. Walirarua kanzu lake. Walichinja mbuzi na kuweka kanzu lake ndani ya damu.
10. Yakobo alifikiria kwamba Yusufu ameuawa na wanyama wakali.

SHULE YA JUMAPILI YA CBM

Awamu ya 1 Mwaka wa 3



9 Yusufu na ndugu zake

Marejeo

Mwanzo mlango wa 37

Kiini cha somo

Kuonyesha matokeo ya chuki na wivu ya ukatili.

Maneno maalum

- 9.1 Yakobo + wana 12 + penda Yusufu zaidi + kanzu ya kipekee + ndugu wana wivu
- 9.2 Yusufu + ndoto + miganda ya nafaka + inamia + jua, mwezi na nyota + inamia + ndugu wanachukia
- 9.3 Yakobo + wana 10 + lisha kondoo + tuma Yusufu
- 9.4 Ndugu wanapanga kuuu + Reubeni + shimo + chukua mbuzi + shimoni
- 9.5 Reubeni hakukuweco + wafanya biashara + uza Yusufu + Misri
- 9.6 Reubeni + Yusufu alienda + udhika + ua mbuzi + damu + kanzu + Yakobo + fikiria Yusufu amekufa + huzunika sana

9.1 Yakobo alikuwa na wana kumi na wawili na aliwapenda wote. Lakini zaidi ya wote alipenda Yusufu sana. Yakobo alitengenezea Yusufu kanzu la kipekee la rangi nyingi. Ndugu zake walimwonea wivu kwa sababu baba yao alimpenda zaidi. Walimwonea wivu kwa sababu ya hilo kanzu la rangi nyingi. Hawakumpenda Yusufu kabisa.

9.2 Yusufu alikuwa na ndoto mbili. Aliota kwamba yeye na ndugu zake walikuwa wanavuna nafaka, miganda ya ndugu zake ziliinamia mganda wake wa nafaka. Tena aliota kwamba jua, mwezi na nyota zilimwinamia. Hizi ndoto zilimaanisha kwamba ndugu zake watakuja kumwinamia. Tutaona baadaye vile hizo ndoto zilitimizwa.


Yusufu aliambia ndugu zake hizo ndoto lakini walikasirika sana. Walimwambia kwamba HAWATAMWINAMIA. Walianza kumchukia Yusufu.

9.3 Siku moja Yakobo alituma wanawe wakubwa kumi kupeleka kondoo kwenye kulikuwa na nyasi nzuri. Lakini Yusufu na nduguye mdogo Benyamini walibaki nyumbani.

Ndugu zake walikuwa kondeni kwa muda mrefu. Yakobo alituma Yusufu kwenda kuona kama walikuwa salama na wazima. Yusufu aliondoka kwenda kuwaangalia.

9.4 Ndugu zake walimwona Yusufu akija kwa umbali. Walimchukia sana na walipanga kumuua. Mkubwa wao Reubeni, alikuwa mzuri kuliko wote. Alisema, "Msimuue Yusufu, wacha tumtupe ndani ya hilo shimo mrefu." Reubeni alipanga kuokoa Yusufu kutoka kwa lile shimo baadaye.

Yusufu alipokuja kwa nduguze, aliwasalamia. Yusufu alikasirika na kuogopa sana alipoona ndugu zake kwa uchungu wanachukua kanzu yake ya rangi nyingi. Walimtupa kwenye shimo mrefu. Alilala humo kwa maumivu na uoga.



9.5 Reubeni alienda ng'ambo ingine kupindua kondoo. Alipokuwa angali huko, watu walikuja na ngamia. Walikuwa wafanya biashara wakienda Misri. Ndugu zake waliamua kwamba badala ya kumuua afadhali kumuua kama mtumwa. Kwa hivyo walimuua kwa wafanya biashara.

Hao wandugu waligawana hizo pesa za fedha na wakajifurahisha. Lakini Yusufu alipelekwa Misri nchi ya mbali kutoka nyumbani kwao. Aliuzwa huko kama mtumwa kwa mtu tajiri.

9.6 Reubeni alirudi usiku na kwenda kwa shimo ili amuokoe Yusufu. Alipopata shimo wazi, alikimbia kwenda kuuliza wenzake nini imefanyika kwa Yusufu. Alikasirika sana aliposikia kwamba Yusufu ameuzwa kama mtumwa.

Kesho yake, hao wandugu waliuua mbuzi na kumwaga damu kwa kanzu yote ya Yusufu ya rangi nyingi. Walipoenda nyumbani walionyesha Yakobo hiyo kanzu. Alifikiria kwamba lazima Yusufu aliuawa na mnyama mkali. Yakobo alikuwa na huzuni sana sana kwa sababu alifikiri mwanawe Yusufu alikuwa amekufa.